

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA TANO

29 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 29 APRILI, 2022

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

WAZIRI WA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja

na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

118. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Magari ya kubeba Wagonjwa katika Vituo Vitatu vya Afya Wilayani Nanyumbu.

119. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaugawa Mkoa wa Tanga ili kuongeza ufanisi katika eneo la Utawala Bora.

120. MHESHIMIWA DAUD PROTAS VENANT (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaigawa Halmashauri ya Wilaya Uyui ili itoe Halmashauri nyingine ya Igalula.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

121. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa nakala ya Sheria ya Maadili kwa Viongozi nchini ikiwemo Wabunge ili kuepuka kukiuka Sheria hiyo.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

122. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa Mradi wa kuzuia mafuriko Mto Msimbazi.

WIZARA YA AFYA:

**123. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Bima za Afya za Wazee ili ziweze kutumika wakiwa nje ya Mikoa ambayo wamepewa Bima hizo.

WIZARA YA KILIMO:

**124. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA
(KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mgambalenga Wilayani Kilolo.

WIZARA YA MAJI:

**125. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY
(MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga mabwawa katika Jimbo la Mbulu Vijijini.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

126. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga gati ya kuegesha Boti na vyombo vya usafiri Bagamoyo ili kuvutia Watalii kutembelea Mbuga ya Saadan.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

127. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ukaguzi wa magari barabarani unahusisha vitu gani.

WIZARA YA NISHATI:

128. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali haioni ni kuwakandamiza Wananchi wa Itigi kwa kuondoa Miji kwenye bei ya kuweka umeme kutoka Shilingi 27,000 hadi 320,000.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MADINI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA
29 APRILI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**